



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



**TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA
MSINGI (PSLE) ULIOFANYIKA SEPTEMBER, 2025**

IMETOLEWA NA:

**KATIBU MTENDAJI
05 NOVEMBA, 2025**

TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) ULIOFANYIKA SEPTEMBER, 2025

1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **168** uliofanyika tarehe **01 Novemba, 2025** katika ofisi za Baraza la Mitihamu la Tanzania zilizopo Dar es Salaam, Baraza la Mitihamu liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Mitihamu wa Kumaliza Elimu ya Msingi uliofanyika Septemba, 2025.

2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

Jumla ya watahiniwa **1,172,324** walisajiliwa kufanya Mitihamu wa Kumaliza Elimu ya Msingi wakiwemo Wasichana **637,162 (54.35%)** na Wavulana **535,162 (45.65%)**. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa wenye mahitaji maalum walikuwa **4,682** sawa na asilimia **0.40**.

Kati ya watahiniwa **1,172,324** waliosajiliwa, watahiniwa **1,146,231** sawa na asilimia **97.77** walifanya mtihamu wakiwemo Wasichana **626,147 (98.27%)** na Wavulana **520,084 (97.18%)**. Aidha, Watahiniwa **26,093 (2.23%)** hawakufanya Mitihamu, kati yao Wavulana ni **15,078 (2.82%)** na Wasichana ni **11,015 (1.73%)**.

3.0 MATOKEO

3.1 Ufaulu wa Jumla

Jumla ya watahiniwa **937,581** sawa na asilimia **81.80** ya watahiniwa **1,146,164** wenye matokeo ya Mitihamu wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2025 wamefaulu kwa kupata madaraja ya **A, B** na **C**. Mwaka 2024 watahiniwa waliofaulu walikuwa asilimia **80.87**. Hivyo, ufaulu wa jumla **umeongezeka** kwa asilimia **0.93**. Kati ya watahiniwa **937,581** waliofaulu, Wavulana ni **429,104** sawa na asilimia **82.51** na Wasichana ni **508,477** sawa na asilimia **81.21**. Mwaka 2024 Wasichana waliofaulu walikuwa asilimia **80.05** na Wavulana waliofaulu walikuwa asilimia **81.85**. Hivyo, ufaulu wa Wasichana **umeongezeka** kwa asilimia **1.16** na ufaulu wa Wavulana **umeongezeka** kwa asilimia **0.66**.

Kuhusu ubora wa ufaulu, watahiniwa **422,923** sawa na asilimia **36.90** wamepata madaraja ya **A** na **B** ikiwa ni ongezeko la asilimia **1.07** ikilinganishwa na mwaka 2024.

Ubora wa ufaulu kwa Wasichana umeongezeka kwa asilimia **0.70**, ambapo mwaka 2025 umefikia asilimia **33.71** ikilinganishwa na asilimia **33.01** mwaka 2024. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa ufaulu katika madaraja ya juu, ambapo daraja la **A** limeongezeka kwa asilimia **0.39** na daraja la **B** kwa asilimia **0.31** ikilinganishwa na mwaka 2024.

Kwa upande wa Wavulana, ubora wa ufaulu nao umeongezeka kwa asilimia **1.52** hadi asilimia **40.73** ikilinganishwa na asilimia **39.21** mwaka 2024. Ongezeko la ubora wa ufaulu limechangiwa na kuimarika kwa ufaulu katika daraja la **A** kwa asilimia **0.78** na daraja la **B** kwa asilimia **0.74** ikilinganishwa na mwaka 2024.

Mchanganuo wa ufaulu katika madaraja mbalimbali umeainishwa katika **Jedwali Na.1.**

Jedwali Na.1: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja

Daraja	Mwaka	Wavulana		Wasichana		Jumla	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
A	2024	52,111	9.50	45,531	6.94	97,642	8.11
	2025	53,484	10.28	45,924	7.33	99,408	8.67
B	2024	163,010	29.71	171,037	26.07	334,047	27.73
	2025	158,349	30.45	165,166	26.38	323,515	28.23
C	2024	233,936	42.64	308,604	47.04	542,540	45.04
	2025	217,271	41.78	297,387	47.50	514,658	44.90
A- C	2024	449,057	81.85	525,172	80.05	974,229	80.87
	2025	429,104	82.51	508,477	81.21	937,581	81.80
D	2024	89,640	16.34	122,995	18.75	212,635	17.65
	2025	81,311	15.64	110,450	17.64	191,761	16.73
E	2024	9,948	1.81	7,892	1.20	17,840	1.48
	2025	9,642	1.85	7,180	1.15	16,822	1.47

3.2 Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri

Kati ya shule **19,436** zenye matokeo ya PSLE 2025, shule nyingi ambazo ni **12,224 (62.89%)** zimepata wastani wa Daraja la **C** (utepe wa Njano) ikilinganishwa na madaraja mengine ya ufaulu. Shule zilizopata wastani wa madaraja ya **A** na **B** (Utepe wa Kijani) **zimeongezeka** kwa asilimia **3.78** kutoka idadi ya shule **4,645 (24.54%)** mwaka 2024 hadi kufikia idadi ya shule **5,503 (28.32%)** mwaka 2025. Aidha, shule

zilizopata wastani wa Daraja la **A-C** ni **17,727** sawa na asilimia **91.21**. Mchanganuo wa idadi ya shule katika Makundi ya Umahiri umebainishwa katika **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2025 ikilinganishwa na Mwaka 2024

Daraja	2025		2024	
	Idadi	%	Idadi	%
A [241-300]	1,397	7.19	1,281	6.77
B [181-240]	4,106	21.13	3,364	17.77
C [121-180]	12,224	62.89	12,838	67.81
D [61-120]	1,705	8.77	1,440	7.61
E [0-60]	4	0.02	9	0.05
JUMLA	19,436	100	18,932	100

3.3 Ufaulu wa Watahiniwa Kimasomo

3.3.1 Masomo ya Lugha

Ufaulu wa somo la **Kiswahili** mwaka 2025 ni asilimia **87.57** ukiwa umeongezeka kwa asilimia **0.99** ikilinganishwa na mwaka 2024, Wasichana wamefaulu kwa asilimia **87.98** na Wavulana kwa asilimia **87.08**. Kwa upande wa somo la **English Language** ufaulu ni asilimia **50.11** ambapo umeongezeka kwa asilimia **6.63** ikilinganishwa na mwaka 2024. Wasichana wamefaulu kwa asilimia **49.50** na Wavulana kwa asilimia **50.85**.

Kwa kuzingatia ubora wa ufaulu, somo la **Kiswahili** limeonesha ongezeko la watahiniwa waliopata daraja la **A** na **B** hadi asilimia **59.65** ikilinganishwa na asilimia **53.46** mwaka 2024. Katika somo la **English Language** ubora wa ufaulu umeongezeka kwa watahiniwa waliopata madaraja ya **A** na **B** hadi asilimia **20.95** kutoka asilimia **15.25** mwaka 2024.

3.3.2 Masomo ya Sayansi Jamii

Ufaulu wa somo la **Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** mwaka 2025 ni asilimia **70.29** na ufaulu wa somo la **Uraia na Maadili** ni asilimia **86.37**. Ufaulu wa **Uraia na Maadili** umeongezeka kwa

asilimia **6.69** ikilinganishwa na mwaka 2024, wakati ufaulu wa **Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** umepungua kwa asilimia **11.62**. Kwa kuzingatia jinsia, Wasichana katika somo la **Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** wamefaulu kwa asilimia **67.17**, huku Wavulana wakiwa na ufaulu wa asilimia **74.06**. Katika somo la **Uraia na Maadili**, Wasichana wameonesha ufaulu wa juu zaidi wa asilimia **86.77** ikilinganishwa na Wavulana ambao ufaulu wao ni asilimia **85.89**. Hivyo, katika somo la **Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** Wavulana wamefaulu zaidi kuliko Wasichana kwa asilimia **6.89** na katika somo la **Uraia na Maadili** Wasichana wamefaulu zaidi kuliko Wavulana kwa asilimia **0.88**.

Kwa ubora wa ufaulu, somo la **Uraia na Maadili** limeonesha ongezeko kubwa la watahiniwa waliopata madaraja ya **A** na **B** kutoka asilimia **46.97** mwaka 2024 hadi asilimia **56.68** mwaka 2025. Hata hivyo, katika somo la **Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi** kumekuwa na kushuka kwa ufaulu wa watahiniwa waliopata madaraja hayo mawili kutoka asilimia **43.59** mwaka 2024 hadi asilimia **27.87** mwaka 2025.

3.3.3 Masomo ya Sayansi na Hisabati

Ufaulu wa somo la **Sayansi na Teknolojia** mwaka 2025 ni asilimia **84.43** ukiwa umeongezeka kwa asilimia **0.68** ikilinganishwa na mwaka 2024. Wasichana wamefaulu kwa asilimia **82.83** na Wavulana kwa asilimia **86.36**. Ufaulu wa somo la **Hisabati** mwaka 2025 ni asilimia **56.66** ukiwa umeongezeka kwa asilimia **1.54** ikilinganishwa na mwaka 2024. Katika somo hili, Wasichana wamefaulu kwa asilimia **54.03** na Wavulana wamefaulu kwa asilimia **59.83**.

Kuhusu ubora wa ufaulu, somo la **Sayansi na Teknolojia** limeonesha **punguo** la watahiniwa waliopata madaraja ya **A** na **B** hadi asilimia **48.14** kutoka asilimia **48.83** mwaka 2024. Katika somo la **Hisabati** ubora wa ufaulu umeshuka hadi asilimia **21.92** kutoka asilimia **22.53** mwaka 2024.

Mchanganuo wa ufaulu wa watahiniwa katika masomo mbalimbali ni kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 3**.

Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu kwa Watahiniwa katika Masomo Mbalimbali

Somo	Mwaka	Idadi	%Waliopata A [41-50]	%Waliopata A hadi B [31-50]	% Waliopata A hadi C [21-50]			%Waliopata D [11-20]	%Waliopata E [0-10]
					Was.	Wav.	Jumla		
Kiswahili	2024	1,204,652	20.58	53.46	86.75	86.39	86.58	12.36	1.05
	2025	1,146,099	24.77	59.65	87.98	87.08	87.57	10.65	1.78
English Language	2024	1,204,600	7.59	15.25	43.37	43.62	43.48	47.01	9.51
	2025	1,146,128	9.12	20.95	49.50	50.85	50.11	36.82	13.07
Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi	2024	1,204,654	9.29	43.59	79.82	84.41	81.91	15.96	2.13
	2025	1,146,135	6.26	27.87	67.17	74.06	70.29	28.17	1.54
Hisabati	2024	1,204,636	7.70	22.53	52.37	58.4	55.12	37.65	7.23
	2025	1,146,128	7.15	21.92	54.03	59.83	56.66	37.30	6.04
Sayansi na Teknolojia	2024	1,204,658	14.22	48.83	82.11	85.72	83.75	13.80	2.45
	2025	1,146,141	17.23	48.14	82.83	86.36	84.43	13.94	1.63
Uraia na Maadili	2024	1,204,644	14.57	46.97	79.62	79.76	79.68	17.48	2.84
	2025	1,146,137	18.25	56.68	86.77	85.89	86.37	10.90	2.73

4.0 MATOKEO YALIYOZULIWA

Baraza la Mitihani la Tanzania **limezuia** kutoa matokeo ya watahiniwa **245** waliopata changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuugua hivyo kushindwa kufanya Mtihani kwa idadi kubwa ya masomo au masomo yote. Watahiniwa husika wamepewa fursa ya kurudia kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) mwaka 2026 kwa mujibu wa Kifungu cha **32(1)** cha Kanuni za Mitihani.

5.0 MATOKEO YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani la Tanzania limefuta matokeo yote ya watahiniwa;

- (a) **31** ambao walibainika kufanya udanganyifu katika Mtihani,
- (b) **07** walioandika lugha ya matusi katika skripti zao.

Matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa Kifungu cha **5(2)(i)** na **(j)** cha Sheria cha Baraza la Mitihani Sura ya **107** kikisomwa pamoja na Kifungu **30(2)(b)** cha Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016.

6.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Jiji, Wakuu wa Shule, Wasimamizi na Wasahihishaji wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, 2025 kwa **kazi kubwa na nzuri** waliyoifanya katika kutekeleza jukumu la Uendeshaji wa Mtihani huo. Aidha, Baraza linawapongeza watahiniwa wote waliofanya Mtihani kwa kuwa na utulivu na kuzingatia taratibu za mitihani katika kipindi chote cha Uendeshaji wa Mitihani.

7.0 UTOAJI WA MATOKEO

Matokeo ya Kumaliza Elimu ya Msingi yalikuwa yakitolewa na kuwekwa kwenye tovuti ya Baraza la Mitihani yakionesha namba na jina la mtahiniwa. Hata hivyo, kwa kuzingatia Kanuni na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, matokeo yatatolewa bila kuwa na majina ya watahiniwa. Namba za mtihani zitatumika kutambua matokeo ya kila mtahiniwa. Hivyo, mtahiniwa atakayesahau namba ya mtihani, mzazi/mlezi anashauriwa kuwasiliana na Mkuu wa Shule ambayo alifanyia Mtihani ili kupata matokeo yake.

8.0 UPATIKANAJI WA MATOKEO

Matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2025 uliofanyika Septemba, 2025 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- www.necta.go.tz,
- www.moe.go.tz
- www.tamisemi.go.tz,

Baraza la Mitihani la Tanzania litawasilisha Matokeo haya kwenye Mamlaka zinazohusika ili zifanye uchaguzi wa watahiniwa wa Kujiunga na Elimu ya Sekondari.



Prof. Said A. Mohamed
KATIBU MTENDAJI

05/11/202

